

Historia fupi ya uhusiano wa Marekani na Hawaii

1826 - Marekani ilitambua ufalme wa Hawaii kama nchi tawala na huru.

1893 - Wanajeshi wa majini wa Marekani waliitwaa Hawaii kwa kisingizio kuwa ilikuwa ni maslahi ya usalama wa Marekani, na Waziri wa Marekani aliinua bendera ya Marekani Hawaii akitangaza kuwa Hawaii ni mahamia ya Marekani. Kisha serikali ya Marekani ilimtoa Malkia Liliuokalani wa Hawaii mamlakani. (Soma kuteta kwa Malkia katika <http://www.kanakamaolipower.org/history.php>).

1898 - Marekani iliambatanisha Hawaii "rasmi," bila kupitia taratibu kama mkataba wa kuambatanisha, hali mikataba aina hiyo yashakuwa yakihitimishwa mapema wakati wa kuambatanisha Louisiana, Florida, Texas, na maeneo mengine. Kwa sheria ya kimataifa ukosefu wa mkataba wa kuambatanisha wamaanisha kuwa uhuru wa nchi iliyoambatanishwa **bado** haijasalimishwa.

1959 - Marekani iliandaa kura ya wazi kuwauliza raia wa Hawaii kama wanataka kuhifadhi hali yao ya mahamia au wanataka kujiunga na Marekani kama jimbo. Kwa maslahi ya matokeo mema kwao waliliacha swali la tatu linaloamriwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa, kama raia wa Hawaii wanataka uhuru. Kwa msaada wa kura zaidi kutoka kwa wafanyi kazi 10,000 wa kijeshi walioko Hawaii walipata kura ya walio wengi kuungana na Marekani halafu wakaijumlisha Hawaii kama jimbo lao la hamsini.

Leo - Hawaii bado ndiyo koloni maridai zaidi ya Himaya ya Marekani, na Marekani bado yawashikilia raia wa Hawaii watafutao uhuru pembeni. Lakini kwa muda gani?

Cha kusikitisha leo, Wamarekani wanaendelea kuonya po pote: "Sisi ndio taifa kuu Duniani!", na nini wanawafunza watoto wao wa shule kusema kwenye Ahadi ya Utii? **"...na uhuru na haki kwa wote!"**

Kujifunza mengi kuhusu harakati za uhuru za Wanahawaii tembelea www.kanakamaolipower.org na www.thelawfulhawaiiangovernment.org

Kutokana na uasi wa Januari 1893, Malkia Liliuokalani, mflame wa kikatiba wa ufalme huru wa Hawaii, alitoa barua hii ya kuteta kwa rais wa Marekani Grover Cleveland, kujadi kuondolewa kwa wanajeshi wa majini wa Marekani wanaowasaidia wahaini kwenye mapinduzi. Mtumo wa makala haya na dua la kumbukumbu la 1897 una athari kwa Sheria ya Umma ya Kimataifa. Inathibitisha kuwa Malkia na wafuasi wake hawakujisalimisha bila masharti kwa serikali ambayo ingeifuata: hivyo kila serikali iliyofuata Hawaii ni serikali isiyolingana na sheria. Serikali ya Haki ya Hawaii daima yahifadhi hadhi yake kama serikali halali. Hii ndiyo barua ya Malkia wetu:

Mimi, Liliuokalani, kwa neema ya Mungu na chini ya katiba ya Ufalme wa Hawaii, Malkia, hapa nateta kwa makini dhidi ya kila tendo na matendo yote yaliyofanywa dhidi yangu na serikali ya kikatiba ya ufalame wa Hawaii na watu wengine wakidai kuanzisha Serikali ya Muda ya na kwa Ufalme huu.

Kuwa nisalimu amri kwa nguvu kuu ya Marekani ambayo Waziri wake wa Kuwakilisha, Mtukufu John L. Stevens, amefanya askari wa Marekani

watue nanga Honolulu na kutangaza kuwa ataunga mkono Serikali ya Muda. Sasa kuepuka mgongano wa vikosi vya silaha, na pengine upotevu wa maisha, nafanya hii chini ya kuteta na nikishurutishwa na hiyo nguvu nakabidhi mamlaka yangu mpaka ule wakati ambao Marekani uta, wakati ukweli utawasilishwa kwake, tengua hatua ya wawakilishi wake na kunirejesha kwa mamlaka ambayo nadai kama mwenye mamlaka ya Visiwa vya Hawaii.

Imefanywa Honolulu hii siku ya 17 ya Januari, A.D 1893.